



LA.235/469/01/34

8 Septemba 2020

**Kwa: Watoa Huduma wote wa Fedha**

**YAH: WARAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA KANZIDATA YA WATOA  
HUDUMA ZA FEDHA NCHINI**

Imetolewa chini ya kanuni ya 40 ya Huduma za Fedha za Kielektroniki ya 2015 ikisomwa pamoja na kifungu cha 56 (3) cha Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015.

Benki Kuu ya Tanzania inatoa taarifa kuwa imekamilisha utengenezaji wa Kanzidata ya watoa huduma za fedha kwa kutumia mamlaka yake chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya 2006 pamoja na Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015. Mchakato wa kuunda kanzidata ulishirikisha taasisi mbalimbali ambazo ni wadau wakuu katika mradi huu na ilifikia kilele kwa uzinduzi wa kanzidata hii ambao ulifanyika tarehe 27 Februari, 2020.

Ili kuweza kufanikisha malengo na uendeshaji wa kanzidata, watoa huduma za fedha wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

**1. Usajili wa Watoa Huduma za Fedha**

- 1.1. Watoa huduma za fedha wote kwa kushirikiana na wasimamizi wao wanatakiwa kujiandikisha kwenye kanzidata hii ndani ya siku 10 kutoka siku ya waraka huu kutolewa.
- 1.2. Mtoa huduma mpya wa malipo, baada ya kupewa leseni na Benki Kuu, anatakiwa mara moja kuomba ruhusa ya kutumia mfumo kutoka kwa Kurugenzi ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Benki Kuu ya Tanzania kwa kutumia fomu inayopatikana kwenye tovuti ([www.fsr.bot.go.tz](http://www.fsr.bot.go.tz)) kwa ajili ya upatikanaji wa haraka.

## **2. Usajili wa vituo vinavyotoa huduma**

Watoa huduma wote wa malipo wanatakiwa kuhakikisha kuwa kituo cha aina yoyote chini ya mamlaka yao ambacho kimetajwa kimeorodheshwa hapa chini, kinasajiliwa kwa kufuata malengo ya uanzishaji wa kanzidata ya watoa huduma za fedha:

- i. Matawi ya benki (benki za biashara)
- ii. Wakala wa benki
- iii. Mashine za kuweka na kutolea fedha
- iv. Wakala wa huduma za fedha kwa simu ya mkononi
- v. Taasisi ndogo za fedha
- vi. Wapokea malipo kwa njia ya benki (kifaa cha malipo)
- vii. Wapokea malipo ya Fedha kwa njia ya huduma ya simu ya mkononi
- viii. Watoa huduma ya bima/madalali/mawakala
- ix. Vyama vya ushirika vya mikopo na akiba
- x. Kifaa cha malipo
- xi. Huduma ya kubadilisha fedha za kigeni
- xii. Madalali wa dhamana
- xiii. Vituo vya matibabu vinavyopokea bima kama vile hospitali, vituo vya afya na maduka ya dawa.
- xiv. Kampuni za fedha na mikopo ya nyumba.

## **3. Taratibu za Usajili**

3.1. Usajili wa kituo chochote utafanyika kupitia programu ya ‘FSR Collect Application’.

Hivyo, mchakato wa kusajili vituo kwa pamoja utafanyika kwa utaratibu na kipindi ambacho kimetengwa na Benki Kuu ili kuhakikisha usawa katika usajili wa awali. Mara tu eneo la kijiografia likishatangazwa kuwa usajili umekamilika, mtoa huduma ya malipo husika atakuwa na jukumu ya kusajili vituo vipya katika eneo hilo.

3.2. Kila kituo kitapatiwa namba ya utambulisho wakati wa usajili, ambayo itaonyeshwa mahali pa wazi ndani ya kituo cha huduma za fedha.

3.3. Mtoa huduma ya malipo atasasisha huduma kwenye kituo kilichosajiliwa kupitia programu ya FSR Collect Application au tovuti ya FSR.

3.4. Mtoa Huduma ya Malipo atasajili au kusasisha taarifa za kituo ndani ya masaa 72 ya kuanzishwa kwa huduma hiyo na atakubali au kukataa huduma zilizosajiliwa kwenye kituo wakati wa usajili wa awali ndani ya siku saba (7)

Watoa huduma ya malipo wanashauriwa kwamba, waraka huu utanza kutumika rasmi kuanzia tarehe ya kuchapishwa.

4. Kwa maelezo zaidi usisite kuwasiliana na Benki Kuu ya Tanzania kupitia anuani ya barua pepe: [FSR@bot.go.tz](mailto:FSR@bot.go.tz).

Dkt. Bernard Y. Kibesse

**Naibu Gavana**

**Uthabiti wa Fedha na Usimamizi wa Benki**